



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na. HWC/L.20/03/VOL VIII/92

11/06/2024

MKURUGENZI MTENDAJI,
KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA (TIC),
S.L.P 938,
DAR ES SALAAM.

YAH: UTAMBULISHO WA KAMPUNI YA C.C.L.E. RUBBER (T) CO. LTD.

1. Tafadhali rejea kichwa cha habari hapo juu.
2. Napenda kukufahamisha kuwa Kampuni ya C.C.L.E. Rubber (T) Co. Ltd ni wamiliki halali wa Viwanja Namba 1- 3 Kitalu V – Chamakweza vyenye ukubwa wa Mita za Mraba 189,116.31 sawa na Ekari 46.73 ambavyo vimepangwa kwa ajili ya Uwekezaji wa Viwanda (Heavy Industry).
3. Kampuni hii ilinunua Ardhi hiyo kutoka kwa wamiliki wa asili na baada ya kununua ilijitambulisha kwenye Kijiji cha Chamakweza kupitia Mkutano Mkuu wa Kijiji wa tarehe 19/03/2024 na kuridhia kuwa Kampuni hiyo imilikishwe eneo hilo kwa ajili ya Uwekezaji.
3. Aidha, baada ya kupata idhini ya Mkutano Mkuu wa Kijiji ya kumilikishwa ardhi hiyo Uliandaliwa Mchoro wa Mipango Miji Na. 19/CHL/529/042024 ambao ulibainisha viwanja vitatu vya matumizi ya Viwanda (Heavy Industry) Viwanja hivyo vilipimwa na kusajiliwa kwa Ramani ya Upimaji Na. E7/40/480 na kupata Viwanja Namba 1 – 3 Kitalu V- Chamakweza.
4. Kwa kuwa, C.C.L.E. Rubber (T) Co. Ltd ni Kamupuni ya kigeni, kwa barua hii nathibitisha kuwa ni wamiliki halali wa Viwanja Namba 1-3 Kitalu V – Chamakweza vyenye ukubwa wa ekari 46.73 na havina mgogoro wowote. Hivyo naitambulisha kwako

S.L.P 65, CHALINZE 114 Barabara ya Morogoro, 61315 Chalinze Pwani . Simu: +023 32935403,
Nukushi: 023 32935402, Barua pepe: dedchalinze@pwani.go.tz Tovuti: www.chalinzedc.go.tz

kwa hatua Zaidi za Umilikishaji kwa Mujibu wa Sheria. Pamoja na Barua hii nimeambatisha pia Certificate of Incorporation, Memorandum and Article of Associations, TIN, Passport za Wakurugenzi wa Kampuni, Mikataba ya kununua Ardhi, Mihutasari ya Serikali ya Kijiji na Mkutano Mkuu wa Kijiji na Ramani ya Upimaji.

5. Naomba kuwasilisha


Salama J. Ndyetabura

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
CHALINZE.**



S.L.P 65, CHALINZE 114 Barabara ya Morogoro, 61315 Chalinze Pwani . Simu: +023 32935403,
Nukushi: 023 32935402, Barua pepe: dedchalinze@pwani.go.tz Tovuti: www.chalinzedc.go.tz